# MNADO NDANI YA QUR_ANI

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

TAHADIY(MNADO) NDANI YA QUR_ANI

Moja katika dalili muhimu nyengine za miujiza ya Qur-ani ni Aya zinzozungumzia na kutoa .mnado

Madhumuni ya aya za tahadiy (mnado)ni aya ambazo zinazungumzia juu ya maadui wanaoupinga uislamu na Qur-ani, aya hizo zinawataka maadui na makafiri kama wanasema kweli walete aya kumi,na kama hawatoweza kuleta aya hizo basi nawalete angalau aya moja -:mfano wa Qur-ani, miongoni mwa aya hizo ni

فَلْيَأْتُوا بِحَدِيثٍ مِّثْلِهِ إِن كَانُوا صَادِقِينَ[1]

Basi nawalete Hadithi kama hizi; ikiwa wanasema kweli (kuwa hii Qur-ani akaitunga Nabii .(Muhammad

قُل لَّئِنِ اجْتَمَعَتِ الإِنسُ وَالْجِنُّ عَلَـي اَن يَأْتُواْ بِمِثْلِ هَـذَا الْقُرْآنِ لاَ يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيراً

Sema “ hata wakijikusanya watu (wote) na majinni ili kuleta mfano wa hii Qur-ani basi .hawangaliweza kuleta mfano wake; hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao

اَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ قُلْ فَأْتُواْ بِعَشْرِ سُوَرٍ مِّثْلِهِ مُفْتَرَيَاتٍ وَادْعُواْ مَنِ اسْتَطَعْتُم مِّن دُونِ اللّهِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ

Ndiyo kweli wanasema kuwa: “Amekitunga mwenyewe (Muhammad kitabu hiki)?” Sema: “Basi leteni sura kumi za uwongo zilizotungwa mfano wa hii, na witeni muwawezao (kuweta) badala .ya Mwenyeezi Mungu (waje wakusaidieni kutunga hivyo) ikiwa mnasema kweli

MAUDHUI YA QUR_ANI

-:Qur-ani nzima inaelezea maudhui ya aina nne

Itikadi: Maudhui ya itikadi yanahusiana na kumuamini Mwenyeezi Mungu, Mitume yake, :1

vitabu vya mitume wake, malaika wake, siku ya kiama, pepo na moto, njia iliyonyooka (haki), .njia isiyonyooka (batili), n.k

Sheria na kanuni: sheria na kanuni zimegawika katika sehemu mbili, nazo ni ibada na :2 .muamala

.Maudhui yanayohusiana na ikhlaki:3

.Visa vilivyo na mafunzo ndani yake :4

.(ISTIKHARA (KUMTAKA MUNGU USHAURI

Hekima za kutumia istikhara ni pale ambapo mwanaadamu anapokuwa anataka kufanya jambo lakini yuko katika hali ya shaka na anataka kufanikiwa katika kulifanya jambo hilo, na hii ni kwa sababu mtu mwenye kufanya jambo akiwa na shaka hawezi kufanikiwa, na kwa sababu .hiyo basi humuomba Mwenyeezi Mungu na kumtaka ushauri ili amsaidie

Jambo la kutaka ushauri kupitia kwa watu wengine kumetiliwa umuhimu mkubwa katika dini ya kiislamu, na katika Qur-ani kuna aya nyingi zinazoelezea kuhusu kutaka ushauri kwa watu wengine. Katika kufanya Istikhara au (kutaka ushauri kwa watu wengine), ni vizuri mwanaadamu baada ya kupata ushauri kupitia kwa wengine kubakia na hiyari katika uamuzi .wake

Surat-Tuuri aya ya 34 [1]

MWISHO